**Learning by Ear**

**People Who Make a Difference**

**HIV-Orphan (Kenya)**

Author: Jan-Philipp Scholz

Editor: Stefanie Duckstein

Proofreader: Tony Dunham

Sound clips in DALET: Learning by Ear-Folder – “LBE_PEO_ORPHAN_O-TÖNE / LBE_PEO_ORPHAN_ATMOS”

CHARACTERS:

Announcer: Female

Sound clips: David Owiti (male, 18 years)
Benson Obudko (male, 70-80 years)
Randiga Eliazar Keya (male, 28 years)
Lorraine Onyango (female, 20 years)

**INTRO (Announcer):**

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga maisha yako. Kwenye mfululizo wa hadithi za “Watu Wanaoleta Mabadiliko” utakutana na mashujaa wa kawaida katika maisha ya kila siku kutoka barani Afrika. Watu hao ni jasiri, wakweli na wamejitolea. Watu hao wana matarajio katika maisha ya baadaye na wanaamini ndoto zao

kuwa zitafanikiwa. Leo hii utakutana na David, kijana yatima mwenye umri wa miaka 18 kutoka nchini Kenya, wazazi wake walifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI.

**TEXT:**

*1. SFX: Opening of goat cage*

*2. Sound Clip David:*
*“Sasa ninawatoa mbuzi kutoka zizini nataka kuwafunga nje pale!”*

*3. SFX: Sounds of goats walking to a place for grazing*

*4. Sound Clip David:*
*“Nikimaliza kazi hii – kinachofuatia ni kutayarisha jembe la ng’ombe. Halafu tutaweza kwenda shambani kulima. Hiyo ndiyo kazi yangu itakayofuata.”*

*5. SFX: Urging of oxen (cattle sounds, cracking of lash etc.)*

*6. Sound Clip David:*
*“Kwa hiyo…. wacha mimi niendelee!”*

*7. SFX: Urging of oxen continued; cock crows*

Ni saa kumi na moja na nusu alfajiri. Kuna giza na kila mtu bado

amelala katika kijiji kidogo cha Alwala huko magharibi mwa Kenya. Naam, sio kila mtu kwa kweli kwa sababu David Owiti tayari ameanza kufanya kazi kwa bidii shambani. Jembe na ng'ombe anavyotumia ni urithi alioachiwa na wazazi wake. Wote wawili walifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI miaka kumi na nne iliyopita.

*8. Sound Clip David:*
*"Kazi yote ninayofanya nilijifunza kutoka kwa babu yangu. Alianza kunifunza kazi hii kutoka mwaka 1999, tulipokuwa tunaishi peke yetu. Nilikuwa namsaidia kufanya kazi hii. Kwa hivyo nilijifunza kidogo kidogo."*

David alikuwa na miaka minne tu wakati wazazi wake walipofariki. Dada yake mkubwa anaitwa Lorraine, na nduguye mdogo wa kiume anaitwa, Benson. Kwa kuwa David ndiye mtoto mkubwa wa kiume katika familia basi ana jukumu maalum la kuwalinda na kuwakimu ndugu zake.

Jambo gumu zaidi, anasema, ni kukusanya fedha za karo kwa ajili ya elimu ya ndugu zake. David ndio kwanza amemaliza elimu yake ya sekondari na angependa kujiunga na chuo kikuu. Lakini kwake nduguze wanachukua nafasi ya kwanza. Anataka kuhakikisha kuwa Lorraine na Benson wote wanapata elimu nzuri kabla ya yeye kuendelea na elimu yake.

*9. SFX: Morning sounds; David taking a bath behind grandfather's*

*shack*

Inaelekea saa moja asubuhi na jua limeanza kuchomoza juu ya kijiji cha Alwala. David naye ndio kwanza amemaliza kazi yake ya shamba. Haraka anaoga nyuma ya kibanda cha babu yake na anajitayarisha kwa kazi yake ya pili. Sio muda mrefu tangu alipoanza kazi ya ualimu katika shule ya msingi ya hapo kijijini. Wakati anatembea mwendo mrefu kuelekea huko shuleni, hupata wasaa wa kuelezea ni kwa nini ana ndoto ya kazi anayoipenda. Anataka kuwa daktari.

*10. SFX: David walking to school*

*11. Sound Clip David (speaking while walking):*
*"Ni kwa sababu ya dhiki nyingi nilizozipitia tangu wazazi wangu walipofariki dunia na sasa ninataka kuwa mtu wa maana. Unajua ukiokoa maisha ya mtu basi watoto hawatapata shida. Wazazi wangu walifariki nilipokuwa mdogo. Nina hamu ya kuwa karibu nao. Kwa hivyo nafikiri nikiweza kuokoa maisha ya mzazi wa mtu basi mtoto wao hatapata shida, hatapitia taabu nilizozipitia mimi."*

Kwa mujibu wa shirika la afya duniani (WHO) takriban watoto milioni 12 wa Kusini ya jangwa la Sahara barani Afrika wameondokewa na mzazi mmoja au wote wawili kutokana na ugonjwa wa UKIMWI – idadi hiyo inaendelea kuongezeka. Wengi kati ya watoto hao wanalazimika kuacha masomo. Wengine wao wanakabiliwa na unyanyapaa katika

jamii. Mayatima ambao hawakubahatika kupata malezi kutoka kwa ndugu na jamaa katika familia huishia maisha ya kurandaranda barabarani – kuomba, kuiba au hata kujihusisha na biashara ya ngono kwa ajili ya kupata fedha.

David anajiona kuwa yeye amebahatika kwa sababu babu na bibi yake wako hai bado. Ni wazee, lakini wanamsaidia kimawazo, mahala pa kuishi na ile hali ya kuwa na uhakika, sio kwake tu bali kwa wajukuu zao wote watatu.

*12. Sound Clip David (speaking while walking):*
*"Katika maisha yangu mtu ambaye ni mfano wa kuiga naweza kusema ni babu yangu. Yeye ndie ambaye kila mara amekuwa akinilea.*

*[Anazungumza kwa Kiluo na rafiki zake aliokutana nao njiani.*
*Speaking in Luo to some friends that he met on the way (15 seconds).]*

*Yeye ndie aliyenilea tangu wazazi wangu walipofariki. Kutoka utoto wangu hadi sasa: Hajanivunja moyo! Sasa amezeeka na amechoka. Kwa hivyo na mimi nataka kuchukua majukumu aliyoyabeba."*

Mbali na kuwalea ndugu zake pamoja na kujitafutia maisha, David anahisi kuwa ni jukumu lake pia kuwarudishia shukurani bibi na babu yake.

Macho ya babu yake hung'ara kwa fahari anapowazungumzia David,

Lorraine and Benson.

*13. Sound Clip Benson Obudko (Luo):*
*"Wajukuu zangu wananisaidia sana maishani mwangu. Mimi niliwasaidia walipokuwa wadogo, na sasa wanarudisha shukurani kwa kunisaidia kadri ya uwezo wao. Mtoto wangu wa kiume alipofariki nilidhani hakutakuwa na mtu wa kunisaidia lakini sasa wajukuu zangu wanafanya kazi nzuri sana. Wanafanya kazi kwa kushirikiana, na wako tofauti sana na vijana wa rika lao. Wana busara sana kwa sababu wao ni yatima na wamepata shida nyingi katika maisha yao."*

Wazazi wa David walipofariki, babu yake alikuwa mgonjwa sana pia. Hata hivyo, anasema wajukuu zake walimuhitaji na hilo lilimpa nguvu mpya ya kupambana na maradhi yake. Hajui ana miaka mingapi lakini uso wake unaonyesha amekula chumvi nyingi yaani anaonyesha kuwa ana umri mkubwa, lakini la muhimu ni kuwa akili yake ni timamu na anafahamu kila kitu vyema.

*14. Sound Clip Benson Obudko (Luo):*
*"Ushauri nitakaowapa ni kuwa wawe na heshima na wafanye bidii kwa ajili ya maisha yao ya usoni. Ninaweza pia kuzungumza nao kwa uwazi juu ya ugonjwa wa UKIMWI. Ninawaasa wajukuu zangu wajikinge. Wasifanye ngono bila kujikinga. Mimi ni mzee ninayeheshimika katika jamii na ninamfundisha kila mtu bila ya uoga."*

*15. SFX: School children playing and waiting for David*

David akifika shuleni, anawakuta watoto wanamsubiri kwa hamu. Ijapokuwa amefundisha katika shule hiyo kwa muda wa miezi michache sasa, David amejijengea uaminifu, heshima na upendo miongoni mwa watoto hao kwa sababu wengi wao wanaishi katika mazingira yanayofanana na ya David, na wanamuona kuwa yeye ni mfano wa kuiga na pia kama kaka yao mkubwa. Randiga Eliazar, msimamizi wake, anashangazwa.

*16. Sound Clip Randiga Eliazar Keya:*
*"Dave ni kijana poa, ni mtu mzuri sana! Sijaona kitu chochote kibaya kwa upande wake tangu alipojiunga nasi. Anapendwa sana. Wakati mwingine akikosa kuja shuleni, watoto wanatuuliza, 'Yuko wapi Mr. David?' wanafunzi wanapenda mtu aliye karibu nao na anayethamini kile wanachokifanya. Kila mara huwashauri wasikate tamaa maishani. Mwaka huu tunao watoto ambao hawana wazazi. Kwa hiyo yeye ni mfano mzuri kwa wanafunzi kwa sababu ana uzoefu huo katika maisha."*

*17. SFX: David teaching in class. We hear him greeting the students and talking about today's lesson: The human body and the blood circulation.*

David anafundisha kila siku kutoka saa tatu asubuhi mpaka saa kumi jioni. Pesa anazopata ni chache – ni chini ya Euro 20 kwa mwezi. Lakini hamu ya kuwaelimisha wanafunzi ndio sababu kubwa inayompa

motisha. Somo la leo ni spesheli na muhimu sana kwa David, kwa sababu linahusu mwili wa mwanadamu na maradhi ya damu.

*18. Sound Clip David:*
*"Katika darasa lile tulikuwa tunajifunza juu ya uzushi na upotofu kuhusu virusi vya HIV na ugonjwa wa UKIMWII. Tuliangalia pia vyanzo na hatua za kujikinga. Kuna watu wanaoamini kuwa UKIMWI haupo. Kuna wengine pia wanaamini kuwa mtu mwenye UKIMWI ni mtu aliyelaaniwa. Na wengine wanaamini eti wale wanaougua UKIMWI labda walikiuka mila katika jamii. Mimi hukasirika! Wanawapotosha watu. Wanawafanya watu wanaougua UKIMWI wanyanyapaliwe na pia kutengwa. Wao ni watu kama sisi!"*

David na ndugu zake hawana virusi vya HIV – tofauti na mayatima wengine ambao wamezaliwa na virusi hivyo vya HIV. Dada yake Lorraine alikaribia kuvipata virusi hivyo pale alipobakwa na mtu aliyejidai kuwa anamsaidia. Hakuambukizwa virusi vya HIV, lakini alipata mimba. Sasa ana jukumu la kumlea mtoto wake mdogo wa kike.

Wakati David akiwa shuleni anafundisha yeye hubakia nyumbani kumlea mwanawe na kufanya kazi za nyumbani kama vile kupika na kufua. Kwa Lorraine, mapambano ya kujitafutia maisha ni magumu mno.

*19. SFX: Lorraine doing some washing in front of the shack*

*20. Sound Clip Lorraine:*

*"Siwezi kusema nina furaha maishani kwa sababu nina shida nyingi sana. Mara nyingine ninakwenda shuleni kwa miguu na nikifika huko sina hata kitu cha kula – Sina hata sabuni ya kuogea!"*

Katika maisha yake magumu, Lorraine anafurahi kuwa na kaka kama David ambaye anajaribu sana kumsaidia kifedha.

*21. Sound Clip Lorraine:*

*"Akipata kitu kidogo anamnunulia ndugu yangu mdogo nguo na mimi pia napata kitu kutoka kwake cha kuendea shule. Yaani anatusaidia sana."*

*22. SFX: David coming back from teaching; starting to take care of the animals straight away*

Ijapokuwa David amemaliza kazi yake ya kufundisha kwa leo, lakini bado hajamaliza majukumu yake. Baada ya mwendo wa nusu saa kurudi kwa babu na bibi yake, lazima achunge ng'ombe. Kazi hii huchukua muda pia pengine mpaka saa kumi na mbili na nusu jioni.

*23. SFX: Cattle grazing, David giving instructions to animals*

*24. Sound Clip David:*

*“Kazi ya kuchunga inachukua muda mrefu. Pengine itanibidi, niifanye mchana kutwa.”*

Pamoja na kuwa analemewa na mzigo mzito wa kazi, David anakubali kuwa anahitaji muda wake binafsi zaidi. Kwa hivyo anajaribu sana kujipa muda wa kupumzika, lakini hiyo si rahisi. Yeye ni binadamu na mara nyingine anataka kufurahi pia kama vijana wengine.

*25. Sound Clip David:*
*“Sio kwamba ninafanya kazi siku nzima siku zote sita katika wiki. Huwa ninapata nafasi siku zingine. Wakati wangu wa mapumziko ninautumia na rafiki zangu, kusoma magazeti na kama kuna mechi ya mpira wa miguu basi mimi hupenda kutazama.”*

Kuna jambo moja ambalo David hakulitaja. Ni kuhusu mtu muhimu katika maisha yake. Mtu ambaye yeye humuendea iwapo mambo yamemzidia – mtu huyo humtia moyo na kumpa nguvu mpya ya kuendelea licha ya wakati mgumu utakaokuwa unamkabili.

*26. Sound Clip David:*
*“Okay, nina mpenzi. Tulikutana nilipokuwa shule ya upili. Yeye alikuwa anasoma kwenye shule iliyo karibu. Tulishirikiana, tulielezana yaliyokuwa yakiendelea katika shule zetu na hivyo ndivyo urafiki wetu ulivyoanza. Sio kitu ambacho kilikuwa kimepangwa.…” (starts to laugh)*

**OUTRO (Announcer):**

Hiyo ilikuwa ni hadithi ya David, kijana yatima mwenye umri wa miaka 18 kutoka Kenya ambaye wazazi wake walifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Licha ya hali ngumu inayomkabili David havunjiki moyo. Juu ya hayo yeye anakubali kuwa hakuna mtu aliye sawa na kisiwa, anafahamu jukumu alilonalo kwa familia yake. Je, wewe unamfikiriaje kijana huyu? Tuandikie maoni yako. Kumbuka unaweza pia kusoma zaidi juu ya makala haya au kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao. Anuani yetu ni www.dw-world.de/lbe

Asante kwa kusikiliza na sina shaka kuwa utajiunga nasi tena katika hadithi nyingine mpya wakati ujao kwenye makala haya ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina “Watu Wanaoleta Mabadiliko”. Hadi wakati ujao, Kwaheri !